African Journal of Advanced Social Sciences

AJASS




Open Access

Check for updates

RESEARCH ARTICLE **Section:** *Literature, Linguistics & Criticism*

# Ulinganishi: Masimulizi Ya Jadi Ya Fasihi Simulizi: Chaka, Sundiata, Liyongo Na Mwindo Na Ya Kisasa

**Martha Nyangweso Syekei**
Chuo Kikuu cha Rongo

## IKISIRI

Fasihi imepitia mabadiliko kadha wa kadha katika hali ya kukua kwake. Mwanzo kulikuwa na fasihi simulizi – hadithi, semi, ngomezi, maigizo, ushairi simulizi na mazungumzo, kisha fasihi hii ikahifadhiwa kimaandishi na kuitwa fasihi andishi – tamthilia, riwaya, hadithi fupi na ushairi andishi. Baadaye fasihi ya kimajaribio imezuka ambayo wengi husema hii kati ya simulizi na andishi na ndiyo imesheheni karne hii mpya – fasihi ya watoto, vijana na watu wazima. Fasihi hii hutumia vigezo mbalimbali vya fasihi simulizi na andishi. Nadharia mbili zilizofaa makala haya ni za uhakiki wa vikale na nadharia ya uamilifu. Mihimili ya nadharia hizi mbili itaonyeshwa jinsi inavyojidhihirisha katika kazi hii ya fasihi. Yaliyomo yatafafanuliwa kwa kuongozwa na nadharia hizi, maelezo na ithibati yatatolewa kwa njia ya maelezo. Matokeo yatadhihirisha namna fasihi imekua na tofauti ya kale na sasa hasa vigezo za vya kutambua mashujaa.

**Maneno Muhimu:** Mighani, shujaa, kale, kisasa, masuala ibuka.

**African Journal of Advanced Social Sciences**

Volume 2, Issue 1, 2026

**ARTICLE HISTORY**

Submitted 21 December 2025

Accepted: 28 December 2025

Published: 20 January 2026

**HOW TO CITE**

Syekei, M. N. (2026). Ulinganishi: Masimulizi Ya Jadi Ya Fasihi Simulizi: Chaka, Sundiata, Liyongo Na Mwindo Na Ya Kisasa. *African Journal of Advanced Social Sciences, 2*(1). Retrieved from https://journals.evonexpublishers.com/index.php/ajass/article/view/61

**Published in Nairobi by Evonex Global, an imprint of Evonex Publishers Limited**

© 2026 The Author(s). This is an open Access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution License (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/), which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium, provided the original work is properly cited.

## Utangulizi

Kila jamii ina mifumo yake teule inayoitambua tofauti na nyingine. Mifumo hiyo mara nyingi huwa mingi kufaidi wanajamii na kusaidia kuendeleza historia kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Baadhi ya mifumo ni kama lugha, chakula, mavazi, dini, ndoa na hata tamaduni. Taasisi mbalimbali hujaribu kuhifadhi mifumo hii katika simulizi au maandishi. Katika karne hii ya ushirini na moja, hifadhi nyingi zimewekwa kimaandishi ili kuwepo kwa muda mrefu iwezekanavyo na la mno wanajamii sasa wana uwezo wa kusoma na kumaizi mambo.

Makala haya yataangazia mashujaa wa kale na walivyo tofauti na wa kisasa. Wanajamii wengi huchukulia kuwa mashujaa wa kale walikuwa zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na lengo lao kuu lilikuwa kutekeleza jukumu fulani, mahsusi kuwakomboa kutoka janga na kuwaongoza kwenye ustawi wa maisha duniani.

Nadharia ya vikale huhusishwa na uhakiki wa tanzu kadhaa za fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Meyer (1993:2010), ruwaza hijirudiarudia na huibua hisia na athari nzito kwenye akili laza ya msomaji wa fasihi.

## Mighani

Wamitila (2005), anasema kuwa mighani ni ngano au hadithi zinazowahusu au zinazozungumzia watu waliotenda matendo ya kishujaa na wanaosifiwa katika jamii fulani. Hizi ni hadithi zinazomhusu mhusika wa kihistoria aliyewahi kuishi. Matukio na matendo ya mhusika huyo yana sifa zinazokiuka uwezo wa kibinadamu. Matendo na matukio yamepigwa chuku ambayo ni mbinu inayotumika kwa mapana. Shujaa huyu na masimulizi kumhusu hubadilishwa kutokana na kuongezwa na mambo mengi yasiyo ya kawaida. Baadhi ya matukio yanayotendeka katika mighani hayawezi kutendeka katika ulimwengu halisi na yanakiuka uhalisi wa kawaida. Nguvu za mashujaa hawa si za kawaida kama kufanya mambo kimiujiza. Ufuatao ni muhtasari wa mashujaa wanne: Sundiata, Mwindo, Shaka na Fumo Liyongo.

## Shujaa Sundiata

Katika jamii ya Mandinga nchini mali huko Afrika magharibi kulikuwa na Sundiata. Sundiata alikuwa mtoto wa mfalme wa nchi. Maisha ya Sundiata hayakufuata mkondo wa maisha ya watoto waliyoyazoea watu wa jamii ile.  Kwa mujibu wa masimulizi ya Sundiata, siku alipozaliwa haikuwa ya kawaida. Anga ilijiengua na nderemo zisizojulikana asili wala fasili kuangua sauti. “Haya tazameni amezaliwa mwanasimba! Mwana wa Nyati amezaliwa!” mjumbe aliyetumwa kwa mfalme alitangaza habari hiyo.

Sundiata alijulikana kama Mwana wa Nyati kwa kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa nembo ya utambulishi wa mamake. Mamake alionekana kwa mara ya kwanza na wawindaji waliokuwa wakipambana na nyati aliyewatafiri watu.  Alikuwa nyati mkali wa kuogofya.  Mfalme alitamwa kutokana na kuzaliwa kwa Sundiata. Mamake Sogolon, naye alikuwa na furaha isiyojua upeo. Hii ilikuwa siku kubwa kwake kwa sababu Sundiata ndiye aliyekuwa mtoto wake wa kwanza.

Maisha ya utotoni ya Sundiata yalizongwa na matatizo chungu nzima. Sundiata hakuweza kusimama na kutembea kama watoto wengine. Mwaka wa kwanza ulipita akitambaa, wa pili na tatu vivyo. Watu walianza kumbeua na kusema kila aina ya maneno. Wengine wakaanza kumpiga vijembe mamake kwa sababu ya mwanawe.  Mke wa kwanza wa mfalme, Sassouma, alimfanyia Sogolon kila aina ya stihizai. Mwanawe aliyejulikana kama Dankarani Tumani, rika moja na Sundiata, alikuwa tayari keshatutumka maungo.

Siku moja Sogolan alikwenda kwa mkemwenza kumwomba viungo vya kuungia chakula. Badala ya kumpa moja kwa moja, Sassouma alianza kumfanyia shokori.  Sogolon alipatwa na uchungu mwingi kutokana na maneno ya Sassouma. Aliporudi nyumbani alikuwa akitokota kwa hasira. Sundiata alitaambua hali ya mamake. Sogolon alisema, “Mwanangu ninachekwa kwa sababu ya hali yako! Sassouma amenifedhehesha kwa kusema mwanawe anao uwezo wa kwenda kumletea majani ya mkuyu kuungia chakula!”

“Mama unataka majani ya mkuyu au mkuyu wenyewe?”  akamwuliza Sundiata.

“Mwanangu, niletee huo mkuyu wenyewe!” alisema Sogolon.

Sundiata alimwagiza mtumishi Fasseke akalete upau wa chuma. Upau ulioletwa uliwachukuwa watu saba kuubeba. Sundiata, aliyekuwa na umri wa miaka saba, aliuchukua ule upau na kuutumia kusimama. Aliposimama upau ulikuwa umepinda na kuchukua sura ya uta. Sogolon alipoona hivyo akaanza kuimba:

*Oh siku iliyoje, siku hii*

*Oh siku ya furaha, siku hii*

*Allah ameiumba siku njema hii*

*Mwanangu anatembea huyu!*

Sundiata alitembea kwa kishindo na kwenda kuung'oa mkuyu ambao aliuleta mbele ya nyumba ya mamake. Watu waliokuwa pale waliachama; wengine walitimua mbio kwa hofu kubwa. Tangu siku hiyo Sassouma naye akaingiwa na gere ya kutaka kumwangamiza Sogolon na mwanawe. Hata hivyo, Sogolon alitumia busara na siku moja usiku yeye na wanawe wote wakaihama nchi ya Mali. Sogolon na wanawe wakiwa uhamishoni, nchi hiyo ilivamiwa na kiongozi katili aliyejulikana kama Saoumaro Kante. Saoumaro alitegemea sihiri kutawala na alikuwa na roho katili kupita kiasi. Pia aliwadhalilisha raia wa Mali. Hata Dankarani Tumani aliishia kutoroka nchi hiyo.

Sasa Sundiata alianza kujiandaa ili kuikomboa nchi yake. Alipata msaada kutoka kwa viongozi kadhaa. Kwa mfano alipewa msaada wa wanajeshi na kiongozi aliyefahamika kama Moussa Tunkara, mfalme wa Mema. Muda si muda Sundiata, mtoto wa Sogolon alirudi kwa kishindo. Bahati mbaya mama mzazi alikuwa amefia ugenini. Saoumaro Kante alikuwa tayari kupambana naye kwa kutegemea nguvu zake za uchawi. Lakini hakuweza kufanikiwa. Sundiata na jeshi lake walifanikiwa kuung'oa utawala katili wa kiongozi huyo na kuanzisha utawala ulioyajali maslahi ya kila raia wa nchi ya Mali. Hakuna kiongozi aliyewahi kuzuka katika nchi ya mali ambaye ana sifa kama za Sundiata. Hata leo watu wangali wanapokezana kisa cha mwana simba Sundiata ambaye wengine wanamwita Sunjata. Sundiata ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa taifa la Mali.

### Shujaa Mwindo

Hadithi hii inasimuliwa kutoka nchi ya Kongo na watu wa kabila la Nyanga. Mwindo ni shujaa aliyezaliwa katika kijiji cha Tubondo kilichotawaliwa na chifu mwovu aliyeitwa Shemwindo. Wazazi wake walikuwa baba Shemwindo na mama Nyamwindo. Shemwindo alikuwa na wake saba na alitoa ilani kwa wake zake kuwa wamzalie wana wa kike tu. Yeyote atakayejifungua mwana wa kiume atauwawa na mwanaye. Wake wa Shemwindo sita wakajifungua watoto wa kike. Wa saba akachelewa na alipofika wakati wa kujifungua mwanawe aliyekuwa wa kiume alitokea kidole cha kati cha mkono. Hata mgao wa kazi Nyamwindo alifanya kwa nguvu japo mjamzito.

Shujaa huyu alikuwa mtoto aliyekuwa na nguvu za kiajabu maana alizaliwa akicheka, akiongea na akitembea. Mkononi alibeba kifaa kinachoitwa Conga mkono wa kulia na shoka mkono wa kushoto. Alivalia bagi mgongoni alikuwa na pepo wa bahati aliyeitwa Kahindo. Shemwindo alipopata habari kuhusu kuzaliwa kwa Mwindo, alifanya juhudi mara tatu kumuua. Mwanzo alimrushia mishale saba lakini ikazuiliwa na nguvu za conga. Pili, Shemwindo alijaribu kumzika Mwindo akiwa hai, Mwindo akatoroka kutoka kaburini. Tatu, shemwindo alimweka Mwindo kwa pipa na kumrusha azame kwa mto. Bahati iliyoje, Mwindo akaogelea na kuenda kwa shangaziye Iyangura.

Kwa shangaziye aliiishi kwa muda na kutimiza masharti ya baba yake kuwa iwapo alitaka amsamehe apande ndizi shamba nzima na kuzivuna siku moja. Hili Mwindo alilitekeleza kwa urahisi na akasamehewa na baba mzazi. Mwindo anarudi kijijini na kujenga madhabahu matatu, moja lake na mengine ya Shemwindo na Iyangura. Lile la Shemwindo likawa kama jela kwa baba mzazi ili ashuhudie jinsi mwindo ni kiongozi bora. Mwindo anateuliwa kuwa chifu anakumbana na hatari lakini kwa sababu ya nguvu za kipekee anawashinda adui wote.

Mwindo ni shujaa anayewaheshimu watu wote katika himaya yake. Ni mpole na mkarimu na aliyejaa ungwana. Anapinga mamlaka ya awali na anasisitiza kuwa wananchi waheshimu mali asilia na wawe na moyo wa kusamehe kila wakati.

### Shujaa Fumo Liyongo

Ni shujaa ambaye asili yake ni pwani ya Afrika Mashariki. Hadithi ya Fumo inasimuliwa na Waswahili wa pwani. Kati ya karne ya tisa hadi kumi na tatu. Kitovu chake asili kilikuwa Pate Shanga. Ni shujaa aliyezuka kutokana na msukosuko wa kivita Afrika Mashariki. Alifanikiwa kuhifadhi utamaduni wa Waswahili. Masimulizi kumhusu yanabadilikabadilika kulingana na jamii zinazioshi eneo la pwani.

Fumo alikuwa shupavu kibiashara na alipozeeka na akafa wasimulizi hueleza kuwa alizika karibu na Mto Ozi, karibu na kisima kule Pate-Kipini. Urithi na mamlaka vilienea katika jamii yake hasa za Afrika Mashariki eneo la pwani. Alizuka kuikomboa jamii kutoka misukosuko ya kivita pamoja na kuwaunganisha wanajamii. Alikuwa stadi kwa kubuni na kutongoa mashairi na nyimbo. Anarejelewa kama Shaha wa Gungu na kadhalika.

Kifo chake Fumo Liyongo kilitokana na kusalitiwa na mwanawe aliyeelezea udhaifu wao. Fumo alidungwa kwenye kitovu kwa msumari akajifia. Hii ni siri iliyojulikana na mama mzazi Mbowe pekee. Fumo aliweza kusukuma mtumbwi kwa mkono kutoka upande mmoja wa mto mpaka upande mwingine. Mtumbwi ulienda kwa nguvu za kusukuma tu. Pia inadaiwa kuwa alimkamata mamba aliyemshambulia mwanamke na kumpasua kinywa.

### Shujaa Shaka

Shaka aliongoza Wazulu na enzi hizo makaburu walikuwa huko. Huyu alikuwa mfalme wa watu wa Zulu kule Afrika Kusini. Wazazi wake walikuwa baba Senzangakhona – mfalme enzi hizo na mama Nandi. Alikuwa pia na shangazi yake aliyeitwa Mkhabayi. Baba yake Shaka alimtesa Nandi – mkewe,ikabidi Nandi ahamie himaya nyingine. Babake Shaka baadaye anakufa Shaka na mama yake wakiwa uhamishoni. Shaka amukua mkubwa pale uhamishini, ambapo anaamua kurejea kwao. Anaandaa jeshi kubwa na kuvamia himaya ya Zulu na kutawazwa mfalme.

Shaka anapanua himaya yake na kuvamia wafalme wa himaya jirani na maeneo yote na kuwaunganisha wawe himaya moja. Nandi aliugua ugonjwa ambao ulimtatiza kwa mwezi mzima na baadaye anakufa na Shaka anaamua kutangaza mwaka mmoja kumwomboleza mama yake. Uchumi unazoroteka na himaya nzima inaporomoka. Nduguye Shaka anayeitwa Dingane na Shangaziye Mhlangana wanapanga njama ya kumwondoa mamlakani. Mshauri mkubwa wa Shaka anakubali njama ya kumuua Shaka. Shaka anauwawa akiwa na kikao na wajumbe. Dingane anachukua hatamu za uongozi ya jamii ya Wazulu.

### Mashujaa Wa Kisasa

Shujaa wa karne hii ya ishirini na moja hawana nguvu za kiajabu kama wale wa kale. Shujaa wa kisasa ni wale wanaopigania mambo yanayokabili dunia kwa njia chanya na wenye nia ya kuleta mabadiliko mazuri kwa wanajamii ka ujumla. Hutetea masuala yanayoibuka katika jamii – masuala nyeti. Suala ibuka ni suala linaloangaziwa na kupewa kipau mbele na jamii. Kwa mfano njaa, kutetea haki za binadamu, ukosefu wa usalama, ugaidi, ugonjwa wa sugu kama kansa na korona, katiba na utekelezaji wake, utunzi wa mazingira na ufanisi wa elimu na teknolojia. Baadhi ya masuala haya ibuka ni ya kisasa na yanaathiri jamii kwa mawanda mapana enzi hizi. Watu ambao wameonekana kubobea katika sehemu moja kwa muda huishia kutambulika kama mashujaa. Mashujaa wa kisasa walihusishwa na kuiangalia miundo ya ndani katika mfumo wa jamii. Kila jamii duniani huwa na mahitaji yake na huwa na taasisi zao za kuyatimiza mahitaji yaliyopo na yanayoibuka katika jamii.

Baadhi ya sifa ambazo hupewa shujaa wa kisasa ni kama:

(a) Vipawa. Wenye talanta zao mara kwa mara wametambulika katika jamii tunamoishi. Mfano wa hawa ni wanaspoti maarufu, wakimbiaji watukuka na wenye kuigiza sarakasi kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Hawa wanatumia vipawa vyao na kuwa wenye manufaa kwa jamii. Mfano ni Eliud kipchoge – mwanariadha aliyekimbia kilomita arobaini na mbili chini ya saa mbili na Usain Bolt aliye na kasi kuu duniani jinsia ya kiume.

(b) Matendo yachekeshayo. Kinaya ni kuwa hata wengine wanaofanya matendo ya kuchekesha sasa wameorodheshwa kama mashujaa. Kwa mfano: '*Githeri man*", huyu bwana alitambuliwa na Raisi Uhuru Kenyatta kwa kula mseto wa mahindi na maharagwe yaliyowekwa ndani ya karatasi ya plastiki wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2017. Alistahimili mlolongo mrefu na jua kali na la kubidi ni kuwa na chakula chake akingoja kutekeleza haki ya kupiga kura. Charles Odongo almaarufu 'Ugali Man' ametambulika kuwa shujaa kwa kurusha ugali na kuishika tena haraka. Sasa amepokea kandarasi na shirika la karata la Odibet ili kuwanasa wa bahati nasibu wengi.

(c) Wanaharakati. Hawa hupigania haki za watu katika jamii hasa watoto, wake na hata wanaume. Katika kategoria hii pia hujumuisha vilema na walio maskini katika jamii. Ukiukaji wa haki za kibinadamu ni jambo ambalo limezua watetezi wa haki na wakati mwingi wanaharakati huchapwa na kuumizwa hata kuuwawa katika harakati za kutetea haki za kimsingi za wenzao. Kwa mfano Profesa Wangari Mathai alituzwa "Nobel Prize' kwa kutetea mazingira na kusaidia kupanda miti mingi nchini Kenya. Hayati Raila Amolo Odinga pia naye amepigania masuala ya demokrasia. Leo hii taifa la Kenya linajivunia kuwa na 'Baba' wa Demokrasia shupavu, jasiri na mweledi RAO.

(d) Wanaofanya matendo ya ukarimu. Pamoja na hawa ni madaktari wanaotafiti na kuvumbua dawa zinazotibu magonjwa. Askari pia wamo kwenye kategoria hii kwa kuipigania amani ndani na nje ya nchi zao. Hawa hujumuisha wale wanaowalea watoto au hata wasiobahatika kifedha katika jamii. Pamoja na watoto na familia za mitaani. Ule uwezo wa kuwapa hata nguo na chakula wakati mwingine hufanya watu kutambulika kama shujaa.

(e) Wafanyabiashara maarufu walio na hela nyingi nchini na duniani. Mara nyingi watu kama hawa hujitolea kujenga miundomsingi kama vyuo au hata hospitali za kusaidia wengi na huishia kutambulika kama mashujaa wa kisasa. Kwa mfano: Bernard Arnault, Bill Gates wa Marekani, Jack Ma wa Uchina, Bezos wa Amazon-Marekani, Manu Chandaria wa Kenya na kadhalika.

(f) Wasomi na wavumbuzi wa dhana au kitu fulani kinacholenga au kitakachosaidia ulimwengu mzima. Ulimwengu sasa unaendelea kwa kasi sana na yeyote anayeufaidi kwa kugundua cha muhimu hutambuliwa na kuwa shujaa. Wengine hutuzwa zawadi spesheli. Kwa mfano: Dada Mariamu kutoka Mombasa sasa ni shujaa wa upishi kwa kupika kwa zaidi ya saa sabini na tano mfululizo. Elon Musk anayetambulika shujaa wa kisasa wa teknolojia duniani yu safu za wavumbuzi tajika.

Hitimisho ni kuna kitabu cha dunia nzima kinachorekodi matendo ya kishujaa na ya kiajabu ambacho huitwa 'Guinness World Record." Kitabu hiki kina rekodi zaidi ya elfu arobaini tangu kuzinduliwa mwaka wa 1955. Baadhi ya matendo ya kishujaa ni walio na nywele ndefu na kucha ndefu duniani.

## Marejeo


Kimani N. & Wafula R. (2002). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. JKF.

TUKI (1981). Kamusi ya Kiswahili Sanifu.  Oxford Publishers.

Wamitila K. (2002). Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila K. (2005). Chemichemi za Kiswahili. Focus Publishers Ltd.

*Wikipedia*. Vitabu vya Mitandaoni.